

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

1.0 Utangulizi

Ndugu Waandishi wa Habari, nimewaita kuzungumzia mambo makubwa matatu:

1. Kwanza, utekelezaji wa Uamuzi wa Serikali kufuatia Uhakiki wa Vyeti vya Kidato cha Nne, Sita na Ualimu;
2. Pili, baadhi ya watu waliojitokeza kujinufaisha na zoezi hili; na
3. Tatu, nitazungumzia kuhusu ajira mpya.

Kama mjuavyo, tarehe 28 Aprili, 2017, Serikali ilitangaza kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa vyeti vya kuhitimu kidato cha nne, cha sita na ualimu kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali na Taasisi za Umma, na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Zoezi la uhakiki wa vyeti kwa watumishi wa Wizara zilizobakia linatarajia kukamilishwa kabla ya tarehe 10 Mei, 2017.

2.0 Utekelezaji wa matokeo ya Zoezi la Uhakiki wa Vyeti vya Kuhitimu Kidato cha Nne, cha Sita na Ualimu

Kama mnavyofahamu, taarifa hiyo ilionyesha kwamba:

- (a) Watumishi **9,932** waligundulika kuwa na vyeti vya kughushi.
- (b) Watumishi **1,538** walikuwa na vyeti vyenye utatata kwa kuwa cheti kimoja kinatumiwa na zaidi ya mtu mmoja.
- (c) Watumishi **11,596** walikuwa na vyeti ambavyo havijakamilika (Incomplete) kwa kuwa wahusika hawakuweza kuwasilisha baadhi ya vyeti/taarifa kwa ajili ya kuhakikiwa kama ilivyoelekezwa.

Kufuatia matokeo haya ya uhakiki, Serikali imeamua wahusika kuchukuliwa hatua zifuatazo:

- (a) Watumishi wote **9,932** ambao wamebainika kuwa na vyeti vya kughushi waondolewe kwenye orodha ya malipo ya mishahara Payrol) na **waachishwe** kazi mara moja kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.
- (b) Watumishi **1,538** wenye vyeti vyenye utata, wanatakiwa kuwasilisha ushahidi wa umiliki wa vyeti hivyo Baraza la Mitihani haraka kabla ya tarehe 15 Mei, 2017. Wakati

watumishi hawa wanaendelea kuthibitisha uhalali wa vyeti vyao, mishahara yao itasimamishwa hadi zoezi hili litakapokamilika.

- (c) Watumishi **11,596** ambao waliwasilisha vyeti pungufu pamoja na wale ambao hawajawasilisha vyeti vyao hadi sasa, wanatakiwa kuwasilisha vyeti hivyo au "Index Numbers" zao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kabla ya tarehe 15 Mei, 2017 kwa ajili ya kuhakikiwa upya.

Aidha, baada ya Taarifa ya matokeo ya uhakiki na uamuzi wa Serikali kutangazwa hadharani, wapo baadhi ya watumishi wamejitokeza na kudai kwamba vyeti vyao ni halali. Watumishi wanaodai kuwa na vyeti halali wanaruhusiwa kukata rufaa kwa utaratibu ufuatao:-

- (a) Waandike barua za kukata rufaa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mara moja. Barua hizo zipitie kwa Waajiri wao na waweke maelezo yao.
- (b) Pamoja na Rufaa za Watumishi hawa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu, UTUMISHI, Waajiri watawajibika kupokea nakala ngumu (hard copy) za vyeti vya wahusika na kuziwasilisha kwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania kupitia anuani yake ambayo ni S.L.P. 2624, DAR ES SALAAM; au nakala laini (soft copy) kwa kutumia barua pepe esnecta@necta.go.tz na pshea@necta.go.tz ili viweze kuhakikiwa upya. Taarifa hii ya nakala laini pia iwasilishwe katika Ofisi ya Katibu Mkuu (Utumishi) kupitia barua pepe ya ps@utumishi.go.tz. Zoezi hili linapaswa kukamilika tarehe 15 Mei, 2017.

3.0 Waliojitokeza Kujinufaisha na Zoezi hili

Jana nimepokea taarifa kutoka kwa baadhi ya Watumishi wenye vyeti feki kwamba wamepigwa simu na maafisa wa Ofisi yetu na wengine Baraza la Mitihani wakidai kwamba wakipewa milioni mbili (2) na wengine milioni tatu (3), watarekebisha taarifa zao. Tumefuatilia majina tuliyopewa, na imedhihirika kuwa watu hao si Watumishi wa Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi wala Baraza la Mitihani la Taifa.

Nataka kuwaarifu waathirika wa zoezi hili kwamba endapo Mtumishi ana cheti halali, hataondolewa katika Utumishi wa Umma. Lakini kama ana cheti feki, ataondoka tu. Hakuna "deal". Napenda pia kuwatahadharisha waathirika kwamba wajihadhari wasije wakaingia kwenye mikono ya matapeli wakapoteza fedha zao.

4.0 Ajira Mpya

- (a) Kama mwendelezo wa Ajira Mpya ambazo Serikali imetoa hadi sasa, Serikali imetoa kibali kuajiri Watumishi wapya 15,000 wa Kada mbalimbali kuanzia leo tarehe 03 Mei, 2017.
- (b) Aidha, Waajiriwa wote lazima vyeti vyao vya elimu na utaalamu vihakikiwe na Mamlaka husika kabla ya kuajiriwa.
- (c) Zoezi la uhakiki limeathiri sana baadhi ya maeneo. Maeneo hayo yatapatiwa Kibali cha Ajira ya dharura, punde watakapowasilisha taarifa za upungufu huo Utumishi.

IMETOLEWA NA:

**OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
NA UTAWALA BORA
03/05/2017**